

Mtanzania uk 8, tarehe 28/01/2019

KANDA

YA ZIWA

MASWA

Wafugaji wamuunga mkono RC

Na SAMWEL MWANGA

WADAU na wafugaji mkoani iyu wameunga mkono kauli Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka kupiga marufuku operesheni ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa wafugaji iliopewa jina la Nzagamba, kuwasaka wahujumu wa sekta ya mifugo na kudhibiti utoroshaji wa mifugo na mazao yake.

Mtaka alionyesha kukasirishwa na kutoridhishwa na utendaji wa watendaji kutoka wizara hiyo ambao wameigeuza operesheni hiyo kuwa kero kwa kuwanyanyasa wafugaji.

Alitoa kauli hiyo Januari 25, mwaka huu mjini Bariadi katika kikao cha viongozi wa Mkoa wa Simiyu na wataalam wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi mbele ya Naibu Waziri, Abdallah Ulega.

Wakizungumza na MTANZANIA kwa nyakati tofauti wafugaji mbalimbali wilayani Maswa ambao pia wamekumbwa na kadhia hiyo, walisema alichokipinga RC Mtaka ndiyo uhalisia na wafugaji wanashindwa kufanya biashara kwa uhuru.

Wakizungumza na waandishi wa habari katika mnada wa Senani ulioko wilayani humo walisema kitendo cha Mtaka

kupiga marufuku utekelezaji wa operesheni hiyo mkoani humo ni sahihi.

Kwa mujibu wa wafugahi hao, watekelezaji wa operesheni hiyo wamekuwa wakiwanyanya wafugaji na kuwapatia usumbufu wa mara kwa mara pindi wanapopeleka mifugo yao kuuzwa kwenye minada.

Mmoja wa wafugaji hao, Masanja Nungha, alisema malengo ya hatua hiyo ni mazuri lakini wameshangaa inatekelezwa ndani ya nchi wakati ilipaswa itekelezwe kwenye mikoa ambayo iko pembezoni mwa mipaka ya nchi yetu. "Hawa

watendaji wa wizara wamekuwa wakitusumbua kweli utakuta umetoa ng'ombe wako zizini nyumbani umeamua kumpeleka mnadani uweze kujipatia fedha kwa ajili ya kuendesha maisha yako.

"Lakini ukikutana nao ni shida kweli, utasumbuliwa kwa kipindi kirefu wakidai kibali wakati natoa ng'ombe wa nyumbani," alisema.

Hivi karibuni Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alifanya ziara ya kazi siku moja mkoani Simiyu, ambako Mtaka alikosoa operesheni hiyo katika mkoa wa Simiyu akisema imekuwa ikiwavuruga wafugaji.

- PICHA: ABDALLAH AMIRI.

TABORA

RC awaonya